

Jina: Nambari:

Sahihi

Tarehe:

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA 2

JULAI/AGOSTI 2014

MUDA: 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO MIGORI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)

102/2

Kiswahili

Karatasi YA 2

Muda: 2 ½

MAAGIZO

- Andija jin alako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- Majiu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili
- Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SEHEMU	ALAMA	TUZO
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Sanaa ya maonyesho ya urembo na mitindo imezidi kukua na kutia for a sana nchini na Afrika kwa jumla katika siku za hivi karibuni. Sanaa hii imebadilika sana kadri ya mpito wa wakati. Kinyume na hapo awali ambapo mashindano ya urembo yalikusishwa uzuri wa sura pekee, katika enzi ya leo, wawaniaji mataji mbalimbali huhitajika kudhihirisha kuwa wana maarifa na hekima ambapo hulazimika hata kueleza jinsi taji fulani wanaweza kulitumia kusaidia jamii iwapo wataibuka washindi.

Vilevile, wanamitindo wamekubali mitindo yenye asili ya Kiafrika na inayoendeleza tamaduni za Afrika, badala ya kuiga mitindo ya kimagharibi. Kwa sasa Kenya na Afrika kwa jumla inajivunia mwigizaji maarufu wa Tuzo ya Oscar, Bi Lupita Nyong'o na mwanamitindo wa kutajika Bi Ajuma. Ufanisi huu haungeweza kufikiwa iwapo Afrika ingeendelea kupapaa na kuiga mitindo ya kimagharibi.

Kwa sasa maonyesho mengi ya urembo na mitindo yanasheni mitindo iiiyosawiri utamaduni wa Kiafrika kama vile matumizi ya khanga, vikoi na lesa katika utengenezaji wa mavazi mbalimbali. Siku hizi tamasha huandaliwa katika shule za upili, vya vikuu na vya vya kiufundi humu nchini kama mbinu ya kukuza vipaji vya wanafunzi.

Katika kongamano la Kimataifa la Ila Ila kuadhimisha miaka 50 ya maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya lililoandaliwa na chama cha Kiswahili cha Taifa, CHAKITA, katika chuo kikuu cha kikatoliki, CUEA, kulibainika kuwepo haja ya sanaa ya mashindano ya urembo na mitindo kusawiri sura kamili ya Kiafrika.

Tamasha za urembo na mitindo zinasheheni vipengele vingi vya fasihi simulizi. Kipera cha fasihi simulizi husheheni sifa mahsusi ambazo hujidhihirisha kupitia tanzu zake anuwai. Fasihi simulizi hubadilika kulingana na mpito wa wakati, maendeleo na mabadiliko ya jamii katika nyanja za kisiasa kijamii na kiuchumi. Katika ulimwengu wa sasa, kuna mambo anuwai yanayoshirikisha wanajamii na yanayosheheni vipengele vya fasihi simulizi. Tamasha za urembo ni miongoni mwa shughuli zinazowakilisha fasihi simulizi ya jadi pamoja na kusawiri hali halisi ya ulimwengu wa sasa.

Baadhi ya sifa katika sanaa ya maonyesho ya mitindo na urembo zinazosawiri sifa za fasihi simulizi ni kama utendaji, hadhira, wahusika na ubunifu. Wanamitindo mbalimbali hupita jukwaani kwa maia na miondoko mbalimbali ili kuonyesha mitindo anuai kama ya mavazi, nywele na urembo. Utendaji ni miongoni mwa sifa muhimu za fasihi simulizi ambapo mtambaji hutumia utendaji iii kuteka hadhira yake na kuwasilisha ujumbe anaokusudia kwa hadhira lengwa.

Tamasha za urembo haziwezi zikafanikishwa bila ya hadhira ambayo ni kiungo muhimu katika mashindano haya. Hadhira hufanikisha tamasha hizi kupitia ada ya kiingilio, kufanya tamasha hizi kufana kwa kushangilia wanamitindo mbalimbali na kuhakiki mitindo na wahusika. Hadhira ni muhimu kwani huwezesha kuchagua washindi na hata kuboresha mitindo kutokana na maoni ya uhakiki wao kwa wasanii. Hii ni sawa na fasihi simulizi, ambapo hadhira ilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuifanikisha.

Wahusika ndio wanaonyesha mitindo mbalimbali ya mavazi au urembo. Kando na kwamba urembo wa wahusika hawa huwa ni kigezo muhimu cha kuamua ufanisi wao katika mashindano hayo, ukamavu wao na ustadi wa miondoko huchangia pakubwa kuboresha tamasha hizi na kuzifanya kuwa za kufana. Bila shaka, fasihi simulizi haiwezi lukami lika bila kuwepo kwa wahusika ambao ni kiungo muhimu katika kipera hiki.

Sharti msanii abuni mitindo mipya na mahsusi iii kuwapiku washindani wake. Mitindo hii huweza kubuniwa kutoka kwa matawi, maua, karatasi na kadhalika almuradi ivutie na kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa kwa hadhira lengwa. Iii kufanikisha hili, mwanamitindo hana budi kuwa na ubunifu wa kiwango chajuu. Aidha fasihi simulizi huhitaji ubunitui katika uwasilishaji wake. Kwa mfano, itahitaji ubunifu wa hail yajuu kusimulia kisa kimoja kwa kutumia mbinu tofauti iii kukifanya kana kwamba kinasimuliwa kwa mara ya kwanza kila wakati mtambaji anaposimulia.

Vilevile, jinsi fasihi simulizi inavyoweza kuhifadhiwa kwa sasa kupitia kanda za video na filamu, tamasha za mitindo zinazohusisha utendaji hai huweza kuhifadhiwa katika video na filamu ambapo hadhira inaweza kurejelea kutazama mashindano hayo. Maleba huhusishwa kupitia mitindo mbalimbali ya mavazi na nywele. Fasihi simulizi vilevile hufanya vivyo hivyo. Hata hivyo tofauti kuu inayojitokeza kati ya fasihi simulizi ya jadi na tamasha za mitindo na urembo ni kwamba, kinyume na fasihi simulizi ambayo ni mali ya jamii, mitindo ya mavazi au nywele ni mali ya mbinu binafsi au aliyebuni ambapo mwenyewe ana haki miliki kisheria.

(Taifa leo, Ijumaa, Februari 21, 2014).

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka (al. 1)

.....
.....

2. Toa tofauti kati ya uhaleki wa wanamitondo wa awali na wa sasa. (al. 2)

.....
.....

3. 'Uafrika unatukuzwa katika maonyesho ya urembo na mitindo' Thibitisha. (al. 2)

.....
.....

4. Lignanisha Fasihi simulizi na sana ya maonyesho ya urembo na mitindo . (al. 6)

.....
.....
.....
.....
.....

5. Taja wanaomiliki

(i) fasihi simuizi (al. ½)

.....
.....

(ii) Sanaa ya maonyesho ya urembo na mitindo (al. ½)

.....
.....

6. Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotumiwa katika taarifa . (al. 3)

(i) Kutia foa

.....
.....

(ii) Kuwapiku

.....
.....

(iii) Maleba

.....
.....

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Waatalamu wa maswala ya kielimu wanadai kuwa huenda nchi hii ikalaumiwa kwa kuendeleza mfumo wa elimu unaozingatia maslahi ya wakwasi na kuwapunza wachochole. Mfumo huu wa elimu umezua mfumo mwingine wa kijamii ambapo watoto wa wenye hadhi wanapata elimu bora kuliko watoto wa maskini. Pengo baina ya haya matabaka linazidi kupanuka kama ardhi na mbingu.

Watoto kutoka jamii hohehahe wanasomea katika shule za umma zisizo na lolote wala chochote na watoto wa kifahari wanasomea katika shule za kibinafsi zilizo na vifaa mufti na mazingira faafu. Mfumo wa jinsi hii ni wa kuitia jamil kitanzi kwa sababu ya kuzuka kwa matabaka yanayohasimiana.

Katika nd-u ambapo asilimia sitini ya watu inaishi katika hali ambayo ni ehini ya dola moja kila siku, watoto wengi huenda shuleni kila kila kula chochote na hushinda hivyo kutwa nzima na wasiamue chochote darasani. Walimu wao nao hawana ilhamu au kariha ya kufanya kazi kwa sababu mazingira ya kikazi ni mabovu na huenda shuleni shingo upande kama wakulima bila pembejeo. Madarasa yao ni mabanda na wengine husomea chini ya miii ambayo inaweza kukatwa wakati wowote na wachorna makaa waliokosana na mazingira. Unapowatazama watoto hawa, kile kinachoitwa sare ya shule kinakirihisha na kuyaudhi macho. Ni matambara yaliyosheheni viraka vya kila ama katika mseto wa ufakiri. Hawa ni wenzetu eti!

Tatizo hili limekuwa nyeti hasa kutokana na utandawazi na mfumo wa soko huru ambao unaruhusu shule za kibinafsi kuendeshwa kama mashirika ya kibiashara. Karo inayolipwa katika shule hizi ni ya kibiashara, majengo na vifaa ni vya kibiashara, walimu ni wa kibiashara, ilimuradi kila jambo lalenga maslahi ya kibiashara ya walala hoi. Hapa ndipo chimbuko la makabila mawili maarufu nchini yaani matajiri walamba vidole na maskini wanaostakimu madongo-kuinama.

Uchunguzi umethibitisha kwamba zaidi ya asilimia sitini ya wanafunzi wanaojiunga na shule za kitaifa hutoka katika shule za kibinafsi zinazomilikiwa na matajiri. Mbinu ya wizara ya Elimu ya kugawa nafasi kwa njia ya haki katika shule za kitaifa haijafua dafu kwa sababu matajiri wajanja huwasajili watoto wao kufanyia mtihani katika shule zisizokuwa na ushindani mkubwa zilizomo mashambani. Kwa kufanya hivyo watoto wa maskini huwa wamefungiwa njia kotekote na kuporwa haki yao. Ama kwa kweli mwenye nguvu mpishe kwani dau la mnyonge haliendijoshi.

Wanafunzi katika shule za kibinafsi hufunzwa katika makundi madogo madogo ambayo humwezesha mwalimu kushughulikia mahitaji ya kibinafsi ya kila mtoto. Wazazi wao pia huwaajiri walimu wakati wa mapumziko iii kugongomeza au kushadidia mada ambazo hawakuzielewa vizuri shuleni. Upeo wa lugha wa watoto hawa hauwezi kulinganishwa na wa wenzao kwa sababu shule zao zina maktaba za kisiasa, vifaa vya kisasa na vitumeme na hufunzwa teknolojia za kileo kuhusu mawasiliano. Watoto hawa huandaliwa ziara za kielirnu iii kutanua uelewa wao wa mambo na vile vile hualikiwa watu wanaosifika katikajamii III kuwahutubia shuieni kwao kuhusu mada mbali mbali. Wawasilishaji hawa huwa ni kielelezo tosha kwa watoto hawa. Mzazi aliyesoma hujua umuhimu wa elimu na hivyo basi huandaa mikakati mahsusi iii kurnfau'lisha mwanawe kinyume na wazazi wakata.

Ni bayana kuwa iwapo hivi ndivyo mambo yalivyo basi hata vyuo vikuu vitakuwa himaya ya watoto wa matajiri huku watoto wa kimaskini wakisubiri kuajiriwa nao kama walinzi na matopasi. Sera za elimu nchini haziwezi kufanikiwa pale ambapo rasilmali muhirnu zinatengewa watu wachache katikajamii. Watoto wa waunda sera hizi husomea katika shule ambazo hufuata mfumo ya kirnataifa ambayo haina mkuruba na yetu hafifu. Katika majukwaa ya kisiasa utawasikia wakisifu mfumo ambao watoto wao wanaukwepa kama ukoma. Imekuja kudhihirika kuwa wale wanaosemekana kuwa viongozi wa kesho ni wale ambao sasa hivi wanasomea katika hizo akadernia na kufuata mfumo ya kigeni au akademia zinazofuata mfumo wetu katika mazingira teule. Swali ni hili, kesho ya mtoto wa kimaskini ni ipi?

Inahitajika mikakati ya kimakusudi iiii kulitanzua swala hii kabla ya milipuko ya kijamii kama vile, ujarnbazi,uuaji, ubakaji, uraibu na mihadarati, na kadhalika. Ipo lazima ya kujenga shule vielelezo katika kila wilaya ambazo zitafadhiliwa na serikali kwa kupewa mahitaji yote muhimu na lazima ya kuanzisha mpango wa lishe bora katika shule iiii kukidhi matilaba ya watoto vote. Udahiti wa wanafunzi katika shule za kitaifa na katika vyuo vikuu ni sharti uvalishwe vazi la utu na uzalendo bila ubaguzi. Shule za umma ziwe na walirnu na madarasa ya kutosha iiii kuondoa matatizo yaliyoibuka kutokana na kuanzishwa kwa mpango wa elirnu ya bure katika shule za msingi. Sera kuhusu shule za chekechea lazirna uzinduliwe kitaifa ili kusawazisha msingi wa kila mtoto kielimu. Waliniu wa shule hizi za malezi lazirna wawe na rnaandalizi sawa yatakayowawezesha kusawazisha viwango kitaalamu. Mitaala yetu ilenge kuzalika kwa binadamu ambaye atajinufaisha yeye binafsi na taifa kwajumla.

Maswali

- (a) Ni mambo yapi muhimu yanayojitokeza katika aya ya tatu hadi ya sabab (maneno 90-100) (ala. 8, 1 utiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- (b) Ni mapendekezo yapi yanayotolewa katika aya aya mwisho (maneno 55- 65) (Alama 7, 1 ya utiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) *Bainisha njia zozote mbili za uanishaji wa irabu huku ikitoa mifano ya irabu hizo.* (Ala. 3)

.....
.....
.....

(b) *Taja hali zozote mbili zinazoweza kufanya kiimbo..* (Ala. 2)

.....
.....

(c) *Bainisha mofimu kaitika neno :* (Ala. 2)

.....
.....

(d) *Tambua viwakifishi vetyenye matumizi yafuatayo:* (Ala. 2)

(i) *Hutumiwa kutenga msemaji na maneno au kauli yake.*

.....
.....

(ii) *Hutoa maelekezo na maagizo katika mazungumuzo na mchezo wa kuiigiza*

.....
.....

(e) *Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha uteuzi.* (Ala. 1)

.....
.....

(f) *Andika kinyume cha senensi ifuatayo :* (Ala. 2)

Mvulana alichafua bendera kisha akaiangua.

.....
.....

(g) *Tumia nomino zifuatazo katika sentensi ili zilite dhana ya maneno yaliyo mabanoni* (Ala. 2)

(i) Uchumi (kielezi)

.....
.....

(ii) mlevi (kivumishi)

.....
.....

(h) **Kanusha kwa umoja bila kutumia 'amba'** (Ala. 2)

Kalamu ambazo zilinunuliwa zimeisha wino.

.....
.....

(i) **Andika kwa usenu halisis:** (Ala. 2)

Mwalimu alimwita Kamau.

.....
.....

(j) **Eleza matumizi matatu ya 'po' katika sentensi ifuatayo.** (Ala. 3)

Alipoumia alipogongwa n hapa, nisipolunyasha hutajua.

.....
.....

(k) **Tunga sentensi moja yenye kirai nomino na kirai kielezi.** (Ala. 2)

.....
.....

(l) **Tofautiasha dhana zifuatazo :** (Ala. 2)

(i) Shamirisho kipozi

.....
.....

(ii) Shamirisho kitondo

.....
.....

(m) **Nyambua vitenzi vifauatavyo katika kauli ulizopewa** (Ala. 2)

(i)Kwa (tendama)

.....
.....

(ii)Suka (Tendata)

.....
.....

(n) **Tunga Sentensi yenye muundo ufauatao :** (Ala. 4)

Nomino + Kishazi tegemezi + Kitenzi + Kielezi

.....
.....

(o) **Andika katika hali ya wastani** (Ala. 2)

Juso la jisichana lile linapendeza

.....
.....

(p) *Tofautisha vitate vifuatavyo :*

(Ala.2)

(i) Ila

.....

(ii) Hila

.....

(q) *Adnika sentensi hii katika wakati usiodhihirika.*

(Ala.2)

Kenya hupokea watali wengi.

.....

.....

(r) *Bainisha maana mbili zinazotokana na sentensi hii.*

(Ala. 2)

DJ alisema atampeleka kwake

.....

.....

(s) *Amrisha katika wingi*

(Ala. 1)

Soma kitabu.

.....

.....

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza umuhimu wa usanifishaji wa Kiwahili.

(Ala.5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Eleza sababu zozote **tano** zinazochangia kufa kwa lugha

(Ala. 5)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....